

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA AMPONGEZA RAIS MAGUFULI KWA KUFANIKISHA HATUA ZA KUANZA KWA UJENZI WA DARAJA LA SELANDER.

Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam napenda kumpongeza Rais wetu Mpendwa Dkt. John Magufuli kwa kufanikisha utilianaji saina Baina ya Serikali ya Tanzania na Korea Kusini kuashiria kuanza kwa ujenzi wa Daraja la Salender litakaloanzia Coco Beach hadi Agha Khan hospital kupitia Bahari ya Hindi ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la msongamano wa magari lililokuwa likipelekea upotevu wa mabilioni ya shilingi.

Rais Dkt. John Magufuli ameamua kutujengea Daraja hili la kisasa baada ya kujionea adha ya foleni inayowasumbua watumiaji wa Daraja lililopo sasa ambalo kimsingi ni finyu na haliwezi kumudu idadi kubwa ya magari yaliyopo sasa.

Mbali na kupunguza foleni ujenzi wa daraja hili la kisasa litasaidia kuboresha mandhari ya Jiji letu la Dar es salaam huku wananchi tukiombwa kuendelea kutoa ushirikiano wakati wote wa ujenzi na kuendelea kuweka jiji letu safi kwani mji wetu Ndio kitovu cha biashara na uchumi wa taifa letu

Ujenzi wa Daraja la Salender utagharimu zaidi ya Shilingi Billion 250 ambapo itachukuwa muda wa miezi 36 hadi kukamilika na litakuwa na urefu wa Km 1.03 kwa upande wa baharini huku likiwa na uwezo wa kuhimili zaidi ya Tani 180 kwa wakati mmoja na magari zaidi ya 55,000 kwa siku.

HAKIKA HUU NDIO UTEKELEZAJI WA YALE ULİYOWAAHIDI WANANCHI KUPITIA ILANI YA CCM.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

23/07/2018